CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# MATUKIO YA MWEZI

OKTOBA HADI DISEMBA, 2019











*"ARDHI NI HAZINA"*

# Jaji Lubuva ataka Taasisi za Elimu ya juu kushirikiana



Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mhe. Jaji Mkuu Mstaafu Damian Lubuva (aliyesimama) akiongea na menejimenti ya SUA

Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mhe. Jaji Mkuu Mstaafu Damian Lubuva amefurahishwa na uhusiano mzuri wa kihistoria na kimaendeleo uliopo kati ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na UDSM.

Jaji Lubuva aliyasema hayo wakati wa ziara yake katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA akiwa ameambatana na Makamau wa Mkuu wa Chuo kikuu ya Dar es salaam Prof. William Anangisye na Maafisa wengine kutoka Chuo hicho kwa lengo la kujifunza na kuendeleza ushirikiano na mahusiano kati ya vyuo hivyo viwili.

"Endeleeni kushirikiana na wenzenu wa vyuo vingine ili kuweza kutatua matatizo yenu kwa ujumla" alisisitiza Mhe.Jaji Mstaafu Lubuva.

Mhe. Lubuva alisema uhusiano mzuri kati ya pande hizo mbili unaleta urahisi wa kushirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali na kujifunza njia bora za kimaendeleo ya Kitaaluma, Miundombinu na Uongozi ambavyo ndio chachu ya maendeleo katika nchi.



Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Prof. William Anangsye

Kwa upande wake Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye alisema SUA ni Chuo ambacho kinatoa watu wenye weledi mkubwa kwenye maswala mbalimbali hususani Kilimo nchini hivyo Chuo Kikuu cha Dar es salaam kinajifunza mambo mengi kutoka SUA.

Pia aliahidi kuajiri wataalamu mbalimbali wanaotoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kwa sababu hana mashaka na uwezo wao.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda alimshukuru Mhe. Jaji Mtsaafu Lubuva kwa kufanya ziara yake chuoni hapo na kuahidi kuendeleza ushirikiano na mshikamano uliopo baina ya pande hizo mbili.



Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda (katikati) aliyevaa miwani akizungumza na Jaji Mstaafu Mhe. Damian Lubuva (wa kwanza kushoto)

# **Waziri Hasunga:** Hongera SUA kwa Elimu na Mbinu bora za Kilimo na Mifugo



*Prof. Raphael Chibunda (wa kwanza kushoto) akimweleza jambo Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga (katikati) alipotembelea SUA*

Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga (MB) amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuwa na utaratibu mzuri wa kutoa Elimu na Mbinu mbalimbali kwa Wakulima wadogo na wakubwa jinsi ya kulima kisasa zaidi ili kufanya Kilimo chenye tija katika safari ya kuelekea Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa kati.

Mh. Japhet Hasunga alisema hayo wakati akifungua siku tatu za Kongamano na Maonesho ya Kilimo na Mifugo lililofanyika kuanzia Jumatano tarehe 3 mpaka tarehe 6 Disemba 2019 kwenye viwanja vya michezo vya Kampasi Kuu SUA.

Alisema kuwa asilimia kubwa ya Watanzania ni Wakulima lakini hawana Elimu sahihi juu ya nini wafanye ili waweze kulima kwa tija, hivyo hatua hiyo inayofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo SUA ni madhubuti na itatufikisha mahali sahihi.

"Naamini kuwa shughuli hii ni utekelezaji wa agizo la Baba wa taifa na Mkuu wa Chuo wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alioutoa wakati akizindua Chuo hiki" alisema Mhe. Hasunga

Nae katibu Mkuu Wizara ya Mifugo Mhe. Elisante Ole Gabriel amesema kwa sasa viwanda vinahitaji rasilimali na mpaka sasa Rasilimali muhimu inayohitajika katika viwanda vya nyama ni kuwa na Mifugo ya kutosha na Tanzania ina mifugo ya kutosha.

Aliongeza kuwa wao kama Wizara ya Mifugo inategema sana Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika kuendeleza shughuli za Mifugo huku akiutaka uongozi wa Chuo kuwaanda wanafuzi kwenda kujiajiri hususani kwenye Sekta ya Mifugo ili kukabiliana na changamoto za ajira zilizopo nchini.

Nae Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia Prof. James Mdoe aliupongeza Uongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) kwa ubunifu mkubwa wanaoufanya katika shughuli mbalimbali hususani za kilimo kwani awali walizoea kuona watu wakijifunza Kilimo Darasani lakini kwa sasa wanajifunza Kilimo Shambani.

Akiongea kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo SUA Naibu Makamu Mkuu wa Chuo taaluma Prof. Peter Gillah alisema kuwa wao kama Chuo wamepokea ushauri na kuahidi kuufanyia kazi huku akiwataka Wanafunzi, Wafanyakazi na Wadau wote kuendelea kutembelea Mabanda mbalimbali katika Maonesho ili kuweza kujifunza zaidi kwani bado kuna siku mbili za maonesho.

# Agenda za Kitaifa za Utafiti wa Mifugo, Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji 2020/ 2025 zazinduliwa SUA

Siku ya Jumamosi tarehe 16 Novemba 2019, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) walizindua agenda za kitaifa za Utafiti wa masuala ya Mifugo, Uvuvi na Ukuzaji Viumbe maji kwa mwaka 2020/2025, tukio ambalo lilifanyika katika ukumbi wa Nelson Mandela Freedom Square, Chuo Kikuu cha Sokoine Kampasi ya Solomon Mahlangu.



*Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mh. Luhaga Mpina (MB) (katikati) wakati alipozindua rasmi agenda za kitaifa za utafiti wa mifugo, uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa mwaka 2020/2025 uliyofanyika SUA Kampasi ya Solomon Mahlangu Mkoani Morogoro mwishoni mwa mwezi Novemba mwaka 2019*

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina (MB) alizindua agenda hizo na kueleza malengo yake ikiwa ni pamoja na kuzifungua tafiti zilizofanyika miaka ya nyuma na kuzifikisha kwa watumiaji, kuweka utaratibu wa kutambua, kuorodhesha na kutumia tafiti zinazofanywa na wanafunzi wa shahada za uzamili, kuweka kanuni zinazotoa muongozo wa utekelezaji wa agenda na kuhakikisha watafiti wanatekeleza wajibu wao na, kuweka utaratibu wa kuwaunganisha Watafiti wa mifugo na uvuvi.

Agenda hizi pia zinalenga kuweka msingi wa kusimamia watafiti kufuatana na mahitaji ya soko na mambo muhimu kitaifa pamoja na kuongeza mnyororo wa thamani kwenye bidhaa za Mifugo na Uvuvi.

Katika tukio hilo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Joelson Mpina (MB) alieleza pia kuwa kwa muda mfupi tangu Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli iingie madarakani imefanikiwa kuongeza kiwango cha ukusanyaji mapato ya sekta ya Mifugo na Uvuvi kutoka billion 21 hadi shilingi bilioni 72.

Alisema kuwa kwa mwaka ujao wa fedha sekta ya Mifugo na Uvuvi inatarajia kuongeza mapato zaidi na kufikia kiasi cha shilingi bilioni 80.

Aidha alisema licha ya ongezeko la mapato, Serikali kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kudhibiti uingizwaji holela wa zao la Mifugo na Uvuvi nchini kitendo kilichokuwa kinapelekea Wafugaji na Wavuvi wa ndani ya nchi kukosa soko na ushindani kukosekana mana wanafuga lakini hawapati soko.

"Nataka niwaambie ya kwamba hadi leo uagizaji wa samaki kutoka nje umeshuka kwa asilimia 67 na mwaka huu tunaoenda hata asilimia 2 haijafika ya kuagiza samaki kutoka nje ya nchi, Hiyo ina maana bilioni 56 zilizokuwa zikitumika na watanzania kuagiza samaki kutoka nje zitatumika hapahapa nchini," alisema Waziri Mpina.

# Prof. Kipanyula: Ubunifu Na Uvumbuzi Ndio Utajili



*Mkurugenzi wa Teknolojia na ubunifu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio Kipanyula (kulia) akikabidhi Cheti kwa Mwanamajalisi*

Mkurugenzi wa Teknolojia na Ubunifu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio J. Kipanyula amesema kuwa Ubunifu na Uvumbuzi ndio utajiri na njia pekee ya kukabiliana na Dunia ya leo ya Sayansi na Teknolojia na ukizingatia tupo katika awamu ya 4 ya Mapinduzi ya Viwanda Duniani.

Prof. Kipanyula aliyasema hayo wakati wa Hafla ya kuwakabidhi Majalisi 165 Tuzo na Zawadi kutokana na umahiri katika Taaluma, Tafiti pamoja na Ushindi wa wavuti Bora katika awamu ya 35 Chuo kikuu Cha sokoine Cha kilimo (SUA) iliyofanyika chuoni hapo siku ya Alhamisi Tarehe 21 Novemba 2019.

Aidha aliongeza kuwa ili kuendana na Wakati tuliopo ni vyema Wakufunzi wa Vyuo Vikuu hususani Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kuandaa Mitaala itakayowafanya Wanafunzi kuwa Wavumbuzi na Wabunifu zaidi na kuachana na Mitaala iliyopitwa na wakati.

"Kama Wakufunzi tunatakiwa kujiuliza je Elimu tuitoayo inawasaidia vijana wetu kufikiria kuwa wabunifu, wavumbuzi na kutambua matumizi sahihi ya teknolojia? Kama tutashindwa kuwekeza kwa vijana hatutafika malengo yetu kwa ujumla" alisema Prof. Kipanyula.

Akizungumza kwa niaba ya Makamu wa Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda, Naibu wa Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Prof. Peter Gillah aliishukuru Wizara ya Elimu kupitia Waziri wake Prof. Joyce Ndalichako kwa Msada wa Fedha zilizosaidia kujenga Mgahawa kwa ajili ya chakula kwa Wanafunzi, ukarabati wa Majengo ya Uandisi pamoja na Hosteli za Nicolus Kuhanga.

Kwa upande wa Prof. John Kesy ambaye alikuwa anakaimu nafasi ya Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo Taaluma wakati wa hafla hiyo, ameelezea jinsi Chuo kinavyotoa uthamani na kuwajali wale wanaofanya vizuri katika masomo yao na kuwashukuru wale wote walijitoa kuweza kuchangia upatikanaji wa zawadi zilizotolewa.

## SUA yapongezwa kwa idadi kubwa ya Wanafunzi wanaojiajiri



*Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobelo*

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobelo amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kwa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa namba moja kwa idadi kubwa ya Wanafunzi wanaojiajiri kutokana na mafunzo wanayopata hususani Wanafunzi kutoka SUA.

Mhandisi Emannuel alisema hayo wakati akifunga siku tatu za Kongamano na Maonesho ya Kilimo na Mifugo yaliyoanza siku ya Jumatano tarehe 3 hadi Ijumaa ya tarehe 6 Disemba 2019 kwenye viwanja vya michezo vya Kampasi Kuu SUA.


“Wiki iliyopita Jumamosi nilikuwa mgeni rasmi kwenye kongamano la wajasiriamali iliyofanyika pale Savoy nilikutana na Wanachuo ambao wanatoka hapa SUA wao wapo kwenye usindikaji walisema sisi tumeamua kuamisha elimu yetu wala sisi hatutaki kuajiriwa na mtu, sisi wale walimu walipotufundisha pale tayari wametuajiri” alisema Mhandisi Kalobelo.

Alisema hotuba ya Baba wa Taifa aliyoitoa wakati wa kuanzisha SUA sasa imeanza kuonekana kwa uhalisia mtaani na kwenye mashamba.

“Kwa hili nawapongeza sana na nimejulishwa kuwa Kongamano limehusisha uwasilishaji wa mada mbalimbali za kitafiti na kitaaluma pamoja na mafunzo ya Wakulima na Wafugaji walioudhuria ili ni jambo jema na linafaa liendelezwe” alisema Mhandisi Kalobelo.

Awali akimkaribisha katibu tawala makamu wa mkuu wa chuo kikuu cha sokoine cha kilimo Prof. Raphael Chibunda alisema kuwa lengo la kufanya kongamano na maonesho ya kilimo kila mwaka ni kuwaleta pamoja Wadau wa sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Misitu ili waweze kujadili na kukubaliana namna wanavyoweza kufanya kazi kwa pamoja ili kuboresha sekta tajwa ili kuweza kuchangia katika pato la taifa.

Alisema kuwa Maonesho hayo hutoa fursa kwa Wafanyakazi na Wanafunzi wa SUA kuonesha Teknolojia pamoja na matokeo ya Tafiti mbalimbali zinazofanywa karibu kila mkoa nchini.



*Tito Siwale (pichani) ni Mhitimu wa SUA akiwa amejiajiri katika Kilimo cha Vitunguu na Pilipili hoho*



# SUA yaendeleza Utamaduni wa Mahafali na Majalisi



*Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda*

Makamu wa Mkuu wa chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda amesema kuwa Chuo hicho kimeendelea kuwa miongoni mwa Vyuo Vikuu Duniani vyenye Utamaduni wa kufanya Mahafali pamoja na Majalisi (Convocation)

Prof. Chibunda alisema hayo wakati akifungua Michezo ya Wanamajalisi wa Chuo hicho yaliyofanyika siku ya Jumatano 20 Novemba 2019 kwenye viwanja vya Kampasi kuu SUA.

"Katika Tamaduni za Vyuo Vikuu vingi Duniani kutokana na kalenda ya Vyuo hivyo, kuna Matukio makubwa mawili ambayo ni Mahafali ya Chuo yanayoambatana na kuwatunuku Shahada na Tuzo mbalimbali Wahitimu pamoja na Majalisi kama maandalizi ya kuwapokea Wahitimu" alisema Prof . Chibunda

Makamuu huyo wa Mkuu wa Chuo aliongeza kuwa Michezo ya Majalisi ni sehemu ya kujenga uhusiano na pia ni sehemu ya maandalizi ya mashindano ya Mashirika ya uma yanayotarajiwa kufanyika mapema Jjijini Mwanza.

Nae Katibu wa Majalisi Prof. Peter Gillah ambaye ni Naibu wa Makamu wa Mkuu wa Chuo taaluma alisisitiza kuwa dhumuni kuu la Bonanza ni kujenga uhusiano baina ya Wanataaluma na wafanyakazi chuoni hapo.



*Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda ( wa 3 kulia aliyeshika mpira) akizungumza na baadhi ya Washiriki wa Bonanza la Michezo wakati wa Ufunguzi wa Bonanza hilo lililofanyka Kampasi Kuu SUA, Novemba, 2019*

# Mhe. Bashe ataka SUA kuzalisha Mbegu bora Nchini



*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (kushoto) wakati wa Ziara yake katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)*

Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe ametoa wito kwa Taasisi mbalimbali nchini ikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,SUA kufanya tafiti zinazoweza kuzalisha idadi kubwa za mbegu bora nchini.

Mhe. Bashe aliyasema hayo wakati akiwa katika ziara yake fupi ndani ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Morogoro tarehe 10 Oktoba 2019.

Mhe. Bashe alisema mbegu zinazotumika nchini asilimia kati ya 60 na 70% zinaagizwa kutoka nchi za kigeni, hivyo hali hiyo inatia hofu kubwa sana katika sekta ya kilimo ambayo ndio ina mchango mama katika pato la taifa nchini.

"Tukiwa tunategemea mbegu kutoa nchi nyingine tunaweza tusipate mbegu zile tunazozihitaji, kwa sababu sisi ndio tunajua hali ya hewa ya nchi yetu," alisema Mhe. Bashe.

Mhe. Bashe alifafanua kwa kina kwa kusema kuwa kilimo kinachangia asilimia 30% GDP nchini huku asilimia 70% ya wananchi wakitanzania wameajiriwa kutokana na sekta ya kilimo.

"Kutokana na kiwango hicho, kuna haja kubwa wataalam kutoka nchini kuweza kufanya tafiti za uzalishaji wa mbegu ili kuweza kuendana na soko husika kuliko kutumia gharama kubwa kwenye uingizaji wa mbegu ambazo zinaweza kuzalishwa nchini". alisema Bashe

Katika ziara hiyo, Mhe. Bashe alisema Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, SUA kina wataalum wengi waliobobea katika maswala ya kilimo, hivyo Chuo hicho kina nafasi kubwa katika kuiendesha sekta hiyo na kuwa kiongozi katika tafiti za kilimo mbalimbali zinazofanyika nchini ili kuweza kuleta chachu na kubadili mtazamo wa kilimo kwa wananchi.



# SUA yawasilisha Mchango wake kwa Serikali



*Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda (wa pili toka kushoto) akikabidhi Hundi ya shiling milioni 100 kwa Waziri wa Fedha Mh. Philip Mpango*

Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kimetoa mchango wa kiasi cha shilingi milioni 100 kwa Serikali katika mwaka wa fedha ulioishia juni 2019.

Hundi (Damy cheque) hiyo ilikabidhiwa na Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo SUA Prof.Raphael Chibunda kwa Waziri wa fedha Mhe. Philip Mpango kwenye hafla iliyofanyika kwenye ukumbi wa Kambarage hazina jijini Dodoma.

Akizungumza mara baada ya kupokea hundi hiyo Waziri Mpango alisisitiza Taasisi za Serikali kutoa gawio na mchango wao kwa Serikali kabla ya kufika tarehe 23 mwezi huu kama agizo la Mhe. Rais alilolitoa hivi karibuni wakati akipokea gawio la Taasisi na mashirika mbalimbali ya Serikali.

Mhe. Waziri alisema Serikali ina taasisi na mashirika 266 na hadi sasa mashirika na taasisi 137 zimeshatoa gawio na michango kwa serikali yenye jumla ya shilingi Trilioni 1.17 huku taasisi na mashirika 129 hayajawasilisha gawio wala mchango wowote kwa serikali.





# SUA Mshindi wa tatu kwenye Hesabu zilizoandaliwa kwa Ubora



*Prof. Raphael Chibunda wa nne toka (kushoto) akipokea Tuzo toka kwa Kaimu Afsa Mkuu Fedha SUA, Petter Willison*

Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimefanikiwa kushika nafasi ya tatu katika Mashindano yanayoandaliwa Mara moja kila mwaka na Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu Kitaifa.

Akizungumza baada ya kukabidhi Tuzo ya kuwa mshindi wa tatu kwa Makamu wa Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda mnamo tarehe 11 Disemba 2019 ofisini kwake, Kaimu Afisa Mkuu fedha SUA Peter Willison amesema kuwa Bodi ya Kitaifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu kila mwaka inaalika Taasisi binafsi pamoja na Mashirika ya Umma kuingia kwenye shindano la kuona Hesabu zilizoandaliwa kwa Ubora wa Viwango vya Kimataifa.

“Hii ni mara ya kwanza kabisa kwa Chuo chetu kushiriki kwenye mashindano haya na kufanikiwa kuwa mshindi wa tatu katika kundi la Taasisi za Umma kwa Elimu ya Juu" alisema Bw. Willison.

Alieleza kuwa Bodi ya Uhasibu ilikuwa inaangalia kama Taasisi zote zilizoshiriki zimefanikiwa kupata zaidi ya asilimia 75 ya maksi walizoziweka na wengine waliokuwa chini ya maksi hawakuweza kuendelea kushindana. Katika tuzo hizo mshindi wa kwanza alikuwa Chuo cha Ustawi wa Jamii, wa pili alikuwa Chuo cha Mzumbe na mshindi wa tatu ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

> “Hii ni mara ya kwanza kabisa kwa Chuo chetu kushiriki kwenye mashindano haya na kufanikiwa kuwa mshindi wa tatu katika kundi la Taasisi za Umma kwa Elimu ya Juu“



# Wahitimu SUA watakiwa kutumia Elimu waliyoipata kujiajiri



Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael T. Chibunda amewataka wahitimu kutumia elimu waliyoipata kuwa Wabunifu, Wajasiriamali na kuzalisha Ajira zao wenyewe ili kujiepusha kuwa wazururaji na walalamikaji mitaani.

Prof. Chibunda alisema hayo wakati wa sherehe za mahafali ya 35 ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo yaliyofanyika siku ya Ijumaa tarehe 22 Novemba 2019 Kampasi ya Solomon Mahlangu Mazimbu.

Aliwasisitiza kuwa kichocheo cha ufanisi,tija na ubunifu katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa ikiwemo uzalishaji mali na kutoa huduma bora kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Kusoma na kufikia hatua ya kutunukiwa Cheti katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Sokoine cha kilimo haijawahi kuwa lelemama basi niombe ridhaa yako ya kuungana na Mwenyekiti wa baraza la Chuo kuwapongeza kwa dhati Wahitimu wote kwa juhudi zao katika masomo zilizowawezesha kuleta mafanikio " alisema Prof. chibunda.

Katika Mahafali hiyo ya Cuo hicho Mkuu wa Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Mhe. Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba aliwatunuku Wahitimu 2876 kwenye fani mbalimbali ambapo kati ya hao wanawake ni 1027 ambao ni sawa na asilimi 35.71, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.5 tofauti na Wahitimu wa mwaka 2018 ambao Wanawake walikuwa ni 874.

Mkuu huyo wa Chuo katika Mahafali hiyo aliwatunuku Wahitimu wa shahada za umahili ambapo kwa upande wa Uzamivu jumla ya Wahitimu 40 waetunukiwa shahada ya Udaktari wa falsafa wanawake wakiwa tisa na wanaume 31, na kwa upande wa wahitimu wa shahada za uzamili jumla ya wahitimu 144 wanawake wakiwa 50 na wanaume 94.

Awali Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman katika hotuba yake alimweleza Mkuu wa Chuo hicho kuwa Baraza hilo limeendelea kutekeleza Majukumu yake kwa Ufanisi mkubwa ili Chuo kitimize Majukumu Makuu ya Chuo ambayo ni kutoa Mafunzo, Kufanya Utafiti, kutoa Huduma za kitaalam na Ugani pamoja na kuzalisha mali.

Majukumu ambayo Baraza limetekeleza ni pamoja na kusimamia na kuidhinisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chuo wa Awamu ya Nne 2016 - 2021 ulioanza kutekelezwa rasmi tarehe 1 Julai 2016, na kwa mwaka wa fedha 2018/2019 utekelezaji wake umekuwa wa asilimia 80.



"Kusoma na kufikia hatua ya kutunukiwa Cheti katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Sokoine cha kilimo haijawahi kuwa lelemama basi niombe ridhaa yako ya kuungana na Mwenyekiti wa baraza la Chuo kuwapongeza kwa dhati Wahitimu wote kwa juhudi zao katika masomo zilizowawezesha kuleta mafanikio "

# SUA, Jeshi la Polisi kuimarisha Ulinzi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimetoa gari kwa kituo kidogo cha polisi SUA kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika maeneo ya Chuo pamoja na jamii inayoizunguka.

Akizungumza wakati akikabidhi gari hilo siku ya tarehe 14 Novemba 2019 Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda ameshukuru Uongozi wa Jeshi Polisi wa Mkoa wa Morogoro kwa kuendelea kuonesha ushirikiano mzuri baina yao na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali ya Chuo hicho.

Prof. Chibunda alisema kuwa gari hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa askari Polisi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi ili kukabiliana na changamoto zilizopo Chuoni hapo na maeneo ya jirani, kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kwa mwaka mpya wa masomo wa 2019 2020 .

"Kwa sasa Chuo kina jumla ya Wanafunzi wapatao 12,300, ambapo ukichanganya na idadi ya Watumishi na familia zao kwa Kampasi zote mbili yani Kampasi kuu na ile ya Solomoni Mahlangu, Chuo kitakuwa na jumla ya wakazi wanaokaribia 17,000, hivyo nina hakika gari hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiusalama. " alisema Prof. Chibunda

Kwa upande wa Naibu makamu mkuu wa chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo utawala na fedha prof. Yasinta Muzanila alisema kuwa wanayo furaha kwa kutimiza ahadi waliyoitoa na kuongeza kuwa licha ya gari hilo kukabidhiwa kwa jeshi la polisi lakini bado ni mali ya SUA na litaendelea kuwa chini ya kituo cha usalama cha chuo hicho.

Akiongea kwa niaba ya Jeshi la polisi, Mkuu wa Kituo cha Polisi cha SUA, Inspekta.Bertha Matiku, Alishukuru Uongozi wa SUA kwa kuwapatia gari hilo na kuahidi kulifanyia kazi kama ilivyokusudiwa.



*Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda (kushoto) akikabidhi funguo ya gari ya doria (inayoonekana pichani) kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi SUA Inspekta Bertha Matiku*


SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE
1984
ARDHI NI HAZINA
CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA)
Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) inawatakiwa wanajumuiya wote wa SUA, na watanzania wote
Heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya.
2020